**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA FEDHA**

**MAMLAKA YA UDHIBITI WA UNUNUZI WA UMMA**
**(PPRA)**

# MWONGOZO WA DHAMANA KATIKA UNUNUZI WA UMMA WA MWAKA 2025.

**MEI, 2025**

***Tarehe ya Kuanza Kutumika: 8 Mei, 2025***

**MWONGOZO WA DHAMANA KATIKA UNUNUZI WA UMMA WA MWAKA 2025.**

| Umeidhinishwa na: | Cheo: | Sahihi: | Tarehe: |
|---|---|---|---|
| Bodi ya Wakurugenzi | Mkurugenzi Mkuu | | 7 Mei, 2025 |

***Umetolewa na:***
*Mkurugenzi Mkuu,*
*Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma,*
*Tambukareli Dodoma,*
*3 Mtaa wa Ununuzi,*
*S.L. P 2865,*
*41104 Dodoma, TANZANIA*
*Barua pepe: dg@ppra.go.tz*
*Simu: +255 (0) 26 296 3854*
*Tovuti: https://www.ppra.go.tz*

**YALIYOMO**

YALIYOMO .......... iii
Chimbuko .......... 1
Wigo .......... 1
Jina la Mwongozo .......... 1
Matumizi ya Mwongozo .......... 1
Maana ya Maneno .......... 2
Madhumuni ya Mwongozo .......... 4
Umuhimu wa Mwongozo .......... 4
Uwasilishaji wa dhamana ya zabuni au tamko la dhaman ya zabuni .......... 4
Aina na Matumizi ya Dhamana ya Zabuni .......... 6
Madai ya Taasisi Nunuzi kwa Kiasi cha Dhamana ya Zabuni .......... 7
Uwasilishaji wa dhamana ya utekelezaji wa mkataba au Tamko la dhamana ya utekelezaji wa mkataba. .......... 8
Uwasilishaji wa Dhamana ya Utekelezaji wa Uhifadhi Mazingira .......... 9
Aina za Dhamana .......... 10
Kazi na Matumizi ya Tamko la Dhamana ya Utekelezaji wa Mkataba .......... 10
Dai la Taasisi Nunuzi .......... 12
Uwasilishaji wa Dhamana ya Malipo ya Awali .......... 13
Matumizi ya malipo ya awali .......... 14
Urejeshaji wa malipo .......... 14
Mapitio ya Mwongozo .......... 15

**TAARIFA ZA UDHIBITI WA NYARAKA.**

| | |
|---|---|
| **Jina la Nyaraka** | Mwongozo wa Dhamana Katika Ununuzi wa Umma wa Mwaka 2025 |
| **Toleo** | Toleo la Pili, Mei 2025 |
| **Nambari ya Nyaraka** | PPRA/PSCD/PSS/25/02 |
| **Jukumu** | Menejimenti, Taasisi Nunuzi |
| **Umeandaliwa na** | Menejimenti |
| **Idhini ya pili (toleo la pili)** | Bodi, Mei 2025 |
| **Matumizi** | Bodi ya zabuni, Kitengo cha Ununuzi na Menejimenti. |
| **Dhumuni** | Kutoa mwongozo kwa Taasisi Nunuzi wakati wa kuamua, kutoa na kusimamia dhamana katika michakato ya zabuni na wakati wa usimamizi wa mkataba |
| **Ni sehemu ya** | Miongozo ya Ununuzi wa Umma. |
| **Nyaraka nyingine zinazohusishwa** | Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura ya 410 na Kanuni za Ununuzi wa Umma Tangazo la Serikali namba 518 la mwaka 2024. |
| **Usambazaji** | Bodi ya Wakurugenzi wa PPRA, Menejimenti ya PPRA, Kitengo cha Usimamizi wa Ununuzi, Taasisi Nunuzi na Afisa Masuuli. |

| SEHEMU YA KWANZA: UTANGULIZI | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | **Chimbuko** | 1.1 | Kwa mujibu wa Kifungu cha 130 cha Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura ya 410 Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) imepewa mamlaka ya kutoa miongozo kwa ajili ya utekelezaji bora wa malengo au majukumu chini ya Sheria. Aidha kifungu cha 67(4) cha Sheria kinaitaka Mamlaka kutoa Mwongozo wa Dhamana katika Ununuzi wa Umma. |
| | | 1.2 | Mwongozo huu umetolewa kwa Taasisi Nunuzi kwa ajili ya kuutumia wakati wa kuamua, kutoa na kusimamia dhamana katika michakato ya zabuni na wakati wa usimamizi wa mkataba. |
| 2. | **Wigo** | 2.1 | Mwongozo huu utatumika kwa Dhamana zifuatazo:<br>a) Dhamana ya Zabuni;<br>b) Tamko la Dhamana ya Zabuni;<br>c) Dhamana ya utekelezaji wa Mkataba;<br>d) Tamko la Dhamana ya utekelezaji wa Mkataba;<br>e) Dhamana ya Uhifadhi wa Mazingira na jamii;<br>f) Tamko la dhamana ya Uhifadhi wa Mazingira na jamii.; na<br>g) Dhamana ya benki kwa malipo ya awali. |
| 3. | **Jina la Mwongozo** | 3.1 | Mwongozo huu utajulikana kama Mwongozo wa Dhamana katika Ununuzi wa Umma. |
| 4. | **Matumizi ya Mwongozo** | 4.1 | Mwongozo huu utaanza kutumika kuanzia tarehe utakaotolewa kwa umma na Mamlaka, na unaweza kufanyiwa marekebisho mara kwa mara pale inapohitajika. |

| | | |
|---|---|---|
| | | 4.2 Mwongozo utatumika na Taasisi Nunuzi zote katika kipindi cha mchakato wa zabuni na usimamizi wa mkataba. |
| | | 4.3 Pale ambapo tafsiri ya kifungu chochote cha Mwongozo huu inaenda kinyume na Sheria ya Ununuzi wa Umma na Kanuni zake, Masharti ya Sheria na Kanuni hizo yatatumika na tafsiri yake itakuwa ya mwisho. |
| 5. | **Maana ya Maneno** | 5.1 Katika Mwongozo huu, isipokuwa pale muktadha utakapohitaji vinginevyo: -<br><br>**Afisa masuuli** maana yake ni afisa wa umma aliyeteuliwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Fedha za Umma au afisa wa umma aliyeteuliwa kwa sheria nyingine yoyote kusimamia fungu au ruzuku na kuwajibika kwa fedha zote zilizotumika kutoka katika fungu hilo au ruzuku.<br><br>**Dhamana ya benki kwa malipo ya awali:** ni aina ya kinga inayoiwezesha Taasisi Nunuzi kurejesha malipo ya awali yoyote yaliyotolewa kwa muuzaji wa bidhaa, mtoa huduma au mkandarasi, pale inapotokea muuzaji atashindwa kufuata masharti na vigezo vinavyosimamia upokeaji, matumizi, na urejeshwaji wa malipo ya awali hayo, katika ununuzi wa bidhaa, huduma au kazi za ujenzi.<br><br>**Mamlaka** maana yake ni Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma.<br><br>**Dhamana ya Utekelezaji wa Mkataba**” maana yake ni dhamana inayotolewa na mzabuni mshindi kwa |

| | | |
|---|---|---|
| | | Taasisi nunuzi kwa lengo la kuhakikisha utekelezaji wa wajibu wa kimkataba.<br><br>**Tamko la Dhamana ya Utekelezaji ya Mkataba:** maana yake ni dhamana kwa njia ya tamko linalotolewa na mzabuni mshindi kwa Taasisi Nunuzi, kwa madhumuni ya kuhakikisha utekelezaji wa wajibu wa kimkataba, ambapo ukiukwaji wa tamko kutokana na kushindwa kwa mzabuni kutimiza wajibu wake au kuvunja masharti ya mkataba chini ya mkataba, utapelekea taratibu za kufungiwa kushiriki zabuni na Mamlaka kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 67 cha Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2023.<br><br>**Dhamana ya Zabuni** maana yake ni dhamana inayotolewa na mzabuni kwa Taasisi Nunuzi kama sehemu ya zabuni yake kwa lengo la kuilinda Taasisi Nunuzi dhidi ya Athari za mwenendo wa mzabuni katika kipindi cha zabuni kwa kuipa haki ya kutaifisha dhamana husika au vinginevyo kurejeshwa kwa mzabuni baada ya kumalizika kwa mchakato wa zabuni.<br><br>**Tamko la Dhamana ya Zabuni** maana yake ni dhamana kwa njia ya tamko linalotolewa na mzabuni kama sehemu ya zabuni yake kwa Taasisi Nunuzi, kwalengo la kuilinda Taasisi Nunuzi dhidi ya hatari ya mwenendo wa mzabuni katika kipindi cha wa zabuni.<br><br>**Dhamana** maana yake ni hati ya dhamana, udhamini au tamko lililowasilishwa na Mzabuni kwa Taasisi Nunuzi kwa madhumuni ya kulinda Taasisi Nunuzi dhidi ya hatari zozote zilizoainishwa au kutambuliwa |

| | | |
|---|---|---|
| | | katika mchakato wa Ununuzi. Dhamana inaweza, pale ambapo imethibitika kwamba Mzabuni amekiuka au ameshindwa kutekeleza masharti ya dhamana hiyo, kutaifishwa na Taasisi Nunuzi au kutekelezwa na mamlaka husika kwa mujibu wa masharti na vigezo vilivyoambatana na dhamana hiyo. |
| 6. | **Madhumuni ya Mwongozo** | 6.1 Kutoa Mwongozo kwa Taasisi za Ununuzi katika umuhimu na matumizi sahihi ya dhamana katika mchakato wa zabuni na usimamizi wa mikataba.<br>6.2 **Dhumuni Mahususi:**<br>Madhumuni mahususi ya Mwongozo huu ni:<br>a) Kutoa utaratibu kwa Taasisi Nunuzi wa namna na wakati wa kutumia dhamana kipindi wa mchakato wa zabuni;<br>b) Kutoa utaratibu kwa Taasisi Nunuzi namna ya kusimamia dhamana katika utekelezaji wa mkataba; na<br>c) Kuhakikisha ulingano wa matumizi ya taratibu na Kanuni za Ununuzi. |
| 7. | **Umuhimu wa Mwongozo** | 7.1 Mwongozo huu utatoa matumizi sahihi ya dhamana katika mchakato wa Ununuzi. |
| **SEHEMU YA PILI: DHAMANA YA ZABUNI NA TAMKO LA DHAMANA YA ZABUNI** | | |
| 8. | **Uwasilishaji wa dhamana ya zabuni au tamko la dhaman ya zabuni** | 8.1 Mahitaji ya kuwasilisha dhamana yatatolewa na Taasisi Nunuzi katika nyaraka ya zabuni, na mahitaji hayo yatatumika kwa wazabuni wote. |
| | | 8.2 Dhamana ya Zabuni au Tamko la dhamana ya Zabuni linapaswa kuwa sehemu ya wasilisho wakati wa kuwasilisha zabuni na mzabuni kabla ya tarehe na wakati wa kufunga. |

| | | |
|---|---|---|
| | | 8.3 Taasisi Nunuzi itabainisha kiasi cha Dhamana ya Zabuni kuanzia asilimia 1.0 hadi asilimia 3.0 ya thamani iliyokadiriwa ya mkataba. Kadiri thamani ya mkataba iliyokadiriwa inavyokuwa ndogo, ndivyo asilimia itakayotumika inavyopaswa kuwa kubwa, na kinyume chake. Taasisi Nunuzi haitatumia asilimia inapohitaji Dhamana ya Zabuni kutoka kwa Wazabuni. Dhamana ya zabuni inapaswa kuoneshwa kwa thamani halisi ya fedha, si kwa asilimia. |
| | | 8.4 Nyaraka za zabuni zitaeleza kwamba mtoaji wa Dhamana ya zabuni na mthibitishaji wake, iwapo yupo, na fomu na masharti ya dhamana ya zabuni vinapaswa vikubaliwe na Taasisi Nunuzi. |
| | | 8.5 Dhamana ya Zabuni au Tamko la dhamana ya Zabuni litasainiwa na kuwasilishwa kielektroniki kupitia mfumo wa NeST pamoja na Zabuni ya Mzabuni kabla ya tarehe na muda wa kufungwa kwa zabuni. |
| | | 8.6 Endapo kunahitajika dhamana ya zabuni, Wazabuni wanapaswa kuwasilisha Dhamana ya Zabuni halisi kabla ya tarehe na muda wa kufungwa kwa zabuni. |
| | | 8.7 Pale ambapo dhamana ya Zabuni ya Kielektroniki inaweza kupatikana moja kwa moja kutoka kwa Mtoaji (kwa mfano, Benki ya Biashara), Dhamana hiyo inaweza kukubaliwa na Taasisi Nunuzi kama nakala halisi ya hati halisi. Jukumu la kuwasilisha Dhamana ya Zabuni kabla ya tarehe na muda wa kufungwa kwa zabuni ni la mzabuni husika. |

| | | |
|---|---|---|
| | | 8.8 Wakati wa kuwasilisha Dhamana ya Zabuni halisi, bahasha ya nje haitapaswa kuwa na jina na anwani ya Mzabuni, bali itakuwa na namba na maelezo ya zabuni husika ili Mzabuni abaki bila kutambulika hadi siku ya ufunguzi wa zabuni. |
| | | 8.9 Taasisi Nunuzi zinatakiwa kuthibitisha uhalali na uhalisi wa dhamana hiyo kwa taasisi/kampuni iliyotoa dhamana mara tu baada ya ufunguzi wa zabuni. |
| | | 8.10 Uthibitisho wa kukubalika kwa mtoaji au mthibitishaji wa dhamana ya zabuni aliyependekezwa haitazuia Taasisi Nunuzi kukataa dhamana ya Zabuni kwa sababu mtoa dhamana au mthibitishaji, kulingana na hali, amefilisika au vinginevyo amepoteza uwezo wa kifedha. |
| 9. | **Aina na Matumizi ya Dhamana ya Zabuni** | 9.1 Taasisi Nunuzi zitawataka wazabuni kuwasilisha pamoja na zabuni zao, kiasi cha Dhamana ya Zabuni au Tamko la dhamana ya Zabuni. |
| | | 9.2 Dhamana ya Zabuni itakuwa katika muundo wa Dhamana ya Benki iliyotolewa na Benki inayotambulika au dhamana ya Bima iliyotolewa na kampuni ya bima inayotambulika. |
| | | 9.3 Dhamana ya Zabuni itaeleza muda wake wa uhalali kama inavyohitajika katika nyaraka za zabuni. Kabla ya kuisha, muda wa uhalali wa dhamana ya zabuni unaweza kuongezwa kwa ombi la Taasisi Nunuzi. |
| | | 9.4 Dhamana ya Zabuni au Tamko la Dhamana ya Zabuni huilinda Taasisi Nunuzi kutokana na |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | kujitoa mapema kwa Wazabuni kwenye mchakato wa zabuni husika. |
| | | 9.5 | Tamko la Dhamana ya Zabuni litatumika kwa ununuzi ambao thamani yake haizidi ukomo wa upendeleo wa kipekee kama ilivyoainishwa katika Majedwali ya Nne (4) na Tano (5) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma, T.S 518 la 2024. |
| | | 9.6 | Tamko la dhamana ya Zabuni linaweza pia kutumika katika ununuzi unaofanywa moja kwa moja kutoka kwa wazalishaji, wakala au wauzaji wa jumla. |
| | | 9.7 | Dhamana ya Zabuni itatumika katika zabuni zote ambazo ziko juu ya ukomo wa upendeleo wa kipekee ulioainishwa katika kifungu cha 9.5 hapo juu. |
| 10. | **Madai ya Taasisi Nunuzi kwa Kiasi cha Dhamana ya Zabuni** | 10.1 | Dhamana ya zabuni au tamko la dhamana ya zabuni litaendelea kuwa halali kwa muda usiopungua siku ishirini na nane zaidi ya muda wa uhai wa zabuni, ili kuipa taasisi nunuzi muda wa kuchukua hatua kama dhamana itaitishwa. |
| | | 10.2 | Endapo Mzabuni atachagua kujiondoa kwenye mchakato wa zabuni mapema kabla ya kusaini mkataba wa ununuzi, Dhamana yake ya Zabuni itataifishwa. |
| | | 10.3 | Pale ambapo Tamko la Dhamana ya Zabuni liliwasilishwa, Mzabuni atawajibika kwa hatua zilizotolewa chini ya tamko hilo ikiwa ni pamoja na kufungiwa kushiriki katika zabuni zinazotangazwa na Serikali kwa kipindi kitakachoamuliwa na Mamlaka kwa mujibu wa Kifungu cha 72 cha Sheria ya Ununuzi wa Umma. |

| | | |
|---|---|---|
| | | 10.4 Taasisi Nunuzi haitadai kiasi cha dhamana ya zabuni, na itarejesha mara moja nyaraka ya dhamana ya zabuni iliyotolewa, baada ya kutokea lolote kati ya yafuatayo:<br><br>a) kumalizika kwa muda wa dhamana ya zabuni;<br>b) kuanza utekelezaji wa mkataba wa ununuzi na uwasilishaji wa dhamana ya utekelezaji wa mkataba ikiwa nyaraka za zabuni inahitaji uwepo wa dhamana;<br>c) kukataliwa kwa zabuni zote na Taasisi Nunuzi kwa mujibu wa Kanuni za Ununuzi wa Umma T.S 518 la 2024; au<br>d) Uondoaji wa zabuni kabla ya tarehe ya mwisho ya kuwasilisha zabuni, isipokuwa kama nyaraka ya zabuni inaeleza kuwa uondoaji huo hauruhusiwi. |
| **SEHEMU YA TATU: DHAMANA ZA UTEKELEZAJI WA MKATABA** | | |
| 11. | **Uwasilishaji wa dhamana ya utekelezaji wa mkataba au Tamko la dhamana ya utekelezaji wa mkataba.** | 11.1 Ndani ya kipindi kilichoainishwa katika nyaraka za zabuni, mzabuni mshindi, baada ya kupokea notisi ya tuzo ya mkataba, atawasilisha kwa Taasisi Nunuzi dhamana ya utekelezaji wa mkataba au tamko la utekelezaji wa mkataba kwa mujibu ya masharti ya mkataba na kwa namna ilivyoainishwa katika nyaraka za zabuni. |
| | | 11.2 Dhamana ya utekelezaji wa mkataba au Tamko la dhamana ya utekelezaji wa mkataba litawasilishwa kabla ya kusainiwa kwa mkataba. Taasisi Nunuzi itahakikisha kwamba Dhamana ya utekelezaji wa mkataba au Tamko la dhamana ya utekelezaji wa mkataba |

| | | |
|---|---|---|
| | | linawasilishwa na mzabuni kabla ya mkataba kusainiwa. Mtumishi yeyote wa Taasisi Nunuzi, ambaye anakiuka sharti hili, atawajibika kwa adhabu kwa mujibu wa Kifungu cha 128 cha Sheria ya Ununuzi wa Umma. |
| | | 11.3 Kiasi cha Dhamana ya Utekelezaji wa mkataba kitakuwa sawa na asilimia kumi (10) ya kiasi cha zabuni kwa Dhamana ya Benki, na asilimia kumi na tano (15) kwa Dhamana ya Bima. |
| | | 11.4 Mzabuni ambaye atashindwa kuwasilisha Dhamana ya Utekelezaji wa mkataba ndani ya kipindi kilichoainishwa ataondolewa sifa ya kusaini mkataba, na mzabuni aliyefuata ataalikwa. Kuondolewa kwa sifa kutakwenda sambamba na kutaifishwa kwa kiasi chake cha Dhamana ya Zabuni au atachukuliwa hatua kwa mujibu wa masharti na vigezo vilivyoelezwa chini ya fomu ya Tamko la Dhamana ya Zabuni iliyowasilishwa na mzabuni. |
| 12. | **Uwasilishaji wa Dhamana ya Utekelezaji wa Uhifadhi Mazingira** | 12.1 Ikiwa Dhamana ya Utekelezaji wa mkataba na Dhamana ya utekelezaji wa uhifadhi wa mazingira zinapaswa kutolewa na mzabuni mshindi,jumla ya dhamana hizo zote mbili hazitazidi asilimia kumi ya bei ya mkataba. |
| | | 12.2 Dhamana ya Utekelezaji wa uhifadhi wa mazingira itahitajika pale ambapo hatari za kimazingira ni kubwa |
| | | 12.3 Iwapo Dhamana ya Utekelezaji wa uhifadhi wa mazingira na jamii itataifishwa na Mwajiri kabla ya kukamilika kwa mkataba, muuzaji wa bidhaa, mtoa huduma au mkandarasi atatakiwa |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | kuwasilisha nyongeza ya dhamana ya utekelezaji wa uhifadhi wa mazingira na jamii ili kufidia kipindi kilichobaki cha mkataba. |
| 13. | **Aina za Dhamana** | 13.1 | Dhamana ya Utekelezaji wa mkataba au Dhamana ya Utekelezaji wa uhifadhi wa mazingira na jamii itakuwa katika mojawapo ya aina zifuatazo:<br><br>a) Dhamana ya Benki isiyo na masharti iliyothibitishwa na benki ya ndani inayotambulika; au ikiwa mzabuni mshindi anatoka nje ya nchi dhamana ya benki itathibitishwa na benki ya ndani; au<br><br>b) Dhamana ya Mdhamini iliyotolewa na mdhamini yeyote anayeheshimika au kampuni ya Bima iliyosajiliwa katika Jamhuri ya Muungano. |
| | | 13.2 | Ikiwa ni Tamko la Utekelezaji wa mkataba, Mzabuni mshindi atajaza na kuwasilisha Tamko lililosainiwa ipasavyo kwa kutumia muundo uliopo katika jedwali la Tatu lililotolewa katika Kiambatisho Na. 1 cha Mwongozo huu bila kufanya mabadiliko yoyote katika maneno yake. |
| | | 13.3 | Ikiwa ni Tamko la Utekelezaji wa uhifadhi wa Mazingira na jamii, Mzabuni mshindi atajaza na kuwasilisha tamko lililosainiwa ipasavyo kwa kutumia muundo uliotolewa katika Kiambatisho Na. 2 cha Mwongozo huu. |
| 14. | **Kazi na Matumizi ya Tamko la Dhamana ya Utekelezaji wa Mkataba** | 14.1 | Tamko la dhamana ya utekelezaji wa mkataba litatumika kwa zabuni zote zenye bajeti zilizo juu ya ukomo wa upendeleo wa kipekee wa kimkoa |

| | | |
|---|---|---|
| | | ulioainishwa katika Majedwali ya Nne na Tano ya Kanuni za Ununuzi ya Umma, 2024 |
| | | 14.2 Tamko la dhamana la utekelezaji wa mkataba litatumika kwa zabuni ambazo ziko chini ya ukomo wa upendeleo wa kipekee wa kimkoa |
| | | 14.3 Baada ya Taasisi Nunuzi kubaini kwamba muuzaji wa bidhaa, mkandarasi, au mtoa huduma amefanya kazi isiyoridhisha, au mzabuni au mshauri elekezi ambaye ameshindwa kutekeleza kwa kuridhisha huduma zinazohitajika chini ya mkataba ndani ya muda uliowekwa, ikijumuisha na nyongeza ya muda ulioongezwa kihalali, kama upo, atawajibika kulingana na masharti na vigezo vya tamko la utekelezaji wa mkataba. |
| | | 14.4 Dhamana ya Utekelezaji wa Mkataba na Tamko la dhamana Utekelezaji wa Mkataba zitatumika kulinda Taasisi Ununuzi kwa kuhakikisha utekelezaji wa mkataba wa muuzaji wa bidhaa, mkandarasi, au mtoa huduma wakati wa utekelezaji. |
| | | 14.5 Dhamana ya Utekelezaji wa Mkataba na Tamko la Utekelezaji wa Mkataba hazitatumika kama mbadala wa kufidia dhima ya kitaaluma inayotokana na uzembe wa kitaaluma, wala bima ya kufidia kitaaluma haitatumika badala ya dhamana ya utekelezaji wa mkataba katika ununuzi wa huduma za ushauri elekezi. |
| | | 14.6 Dhamana ya Utekelezaji wa Mkataba itatumika kama ukomo kwa Taasisi Nunuzi katika kutoza fidia ya ucheleweshwaji wa utekelezaji wa mkataba wa usambazaji wa bidhaa, huduma, au kazi za ujenzi. |

| | | |
|---|---|---|
| | | 14.7 Kiwango cha fidia ya ucheleweshaji wa utekelezaji wa mkataba kitakuwa kati ya asilimia 0.10 hadi 0.20 ya thamani ya mkataba kwa ununuzi wa bidhaa kwa kila siku ya ucheleweshaji. Kwa huduma zisizo za ushauri elekezi, Mtoa Huduma atalazimika kuilipa Taasisi Nunuzi kiasi sawa na asilimia 0.10 hadi 0.20 ya thamani ya mkataba, na kwa kazi za ujenzi, Mkandarasi atalipa kiasi sawa na asilimia 0.10 hadi 0.15 ya thamani ya mkataba kwa kila siku ya ucheleweshaji wa utekelezaji wa mkataba. Kwa huduma za ushauri elekezi, Mshauri elekezi atalazimika kulipa fidia ya aslimia 0.10 hadi 0.20 ya asilimia ya thamani ya mkataba hadi kiwango cha juu cha dhamana ya utekelezaji wa mkataba. |
| | | 14.8 Kwa hali yoyote ile, jumla ya fidia ya ucheleweshaji wa utekelezaji wa mkataba haipaswi kuzidi kiwango cha Dhamana ya Utekelezaji wa Mkataba |
| | | 14.9 Iwapo Tamko la utekelezaji wa mkataba limetumika, kiwango cha fidia ya ucheleweshaji kitakuwa kati ya asilimia 0.10 hadi 0.20 ya thamani ya mkataba, gharama, au thamani ya mkataba wa kazi au huduma kwa kila siku ya ucheleweshwaji, hadi kiwango cha juu cha asilimia 10 ya thamani ya mkataba. |
| 15. | **Dai la Taasisi Nunuzi** | 15.1 Pale ambapo muuzaji wa bidhaa, mkandarasi au mtoa huduma atashindwa kufanya kazi kufikia kiwango kinachotakiwa au atashindwa kutimiza majukumu yake kama ilivyokubaliwa, Taasisi Nunuzi itadai Dhamana ya Utekelezaji wa Mkataba kutoka kwa benki au kampuni ya |

| | | |
|---|---|---|
| | | bima ndani ya muda kwa mujibu wa vigezo na masharti vilivyoainishwa; na kwa upande wa Tamko la Utekelezaji wa Mkataba, Taasisi Nunuzi itaanzisha taratibu za kumfungia mzabuni kama ilivyoelezwa katika Sheria ya Ununuzi wa Umma na Kanuni zake. |
| **SEHEMU YA NNE: DHAMANA YA MALIPO YA AWALI** | | |
| 16. | **Uwasilishaji wa Dhamana ya Malipo ya Awali** | 16.1 Iwapo itahitajika na imeelezwa katika mkataba wa ununuzi, na baada ya kusainiwa kwa mkataba, Muuzaji wa bidhaa, mkandarasi au mtoa huduma atawasilisha kwa Taasisi Nunuzi maombi ya malipo ya awali kwa kutumia fomu maalumu ilivyoainishwa kwenye nyaraka za zabuni. |
| | | 16.2 Kiasi cha Malipo ya awali hakitazidi kile kilichoanishwa kwenye Mkataba |
| | | 16.3 Kiasi cha malipo ya awali kilichokubaliwa kitaelezwa katika nyaraka za mkataba, na kwa namna yoyote hakitazidi asilimia thelathini ya thamani ya mkataba. |
| | | 16.4 Malipo yoyote ya awali yanayozidi asilimia thelathini yatafanyika baada ya kupata idhini ya Mamlaka. |
| | | 16.5 Kabla ya malipo ya awali kufanyika, Taasisi Nunuzi itahakikisha kwamba:-<br>a) Malipo ya awali yanatolewa baada ya kupokelewa dhamana ya Malipo ya awali kutoka benki inayoaminika;na<br>b) uhalali wa dhamana utathibitishwa na benki iliyotoa dhamana hiyo. |
| | | 16.6 Dhamana ya malipo ya awali itabaki kuwa halali hadi pale muuzaji wa bidhaa, mkandarasi, au |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | mtoa huduma atakapokamilisha sehemu ya kazi au huduma zake, au atakapokabidhi bidhaa zinazolingana na thamani ya dhamana ya malipo ya awali iliyotolewa. |
| 17. | **Matumizi ya malipo ya awali** | 17.1 | Malipo ya awali yatatumika kwa ajili ya gharama za awali za mkataba au mradi na hayatazidi kiasi cha maandalizi ya mahitaji au upatikanaji wa mahitaji ya awali kwa kadiri itakavyokuwa imeainishwa kwenye mkataba. |
| | | 17.2 | Muuzaji wa bidhaa, mkandarasi au mtoa huduma hatatumia kiasi cha malipo ya awali kwa kazi nyingine tofauti na kazi zilizoainishwa katika mkataba. Kufanya hivyo Taasisi Nunuzi itakuwa na sababu ya msingi kudai kurejeshewa malipo kutoka kwa mdhamini. |
| 18. | **Urejeshaji wa malipo** | 18.1 | Kiasi cha dhamana ya benki ya malipo ya awali kitapunguzwa kidogo kiodogo kulingana na kiwango cha malipo ya awali kilichorejeshwa na muuzaji wa bidhaa, mkandarasi, au mtoa huduma na Taasisi Nunuzi itahakikisha kuwa kiasi hicho kimekwisharejeshwa kikamilifu pale mkataba unapofikia asilimia themanini ya utekelezaji au malipo. |
| | | 18.2 | Pale ambapo Taasisi Nunuzi itashindwa kurejesha malipo yote ya awali wakati wa utekelezaji wa mkataba kutokana na kutotekelezwa kwa wajibu wa muuzaji wa bidhaa, mkandarasi au mtoa huduma chini ya mkataba, Taasisi Nunuzi itadai kutoka kwa Mdhamini kurejeshewa kiasi cha malipo ya awali kilichobaki kulingana na masharti na vigezo vya mkataba. |

| | | |
|---|---|---|
| | | 18.3 Masharti na vigezo vingine vya dhamana yatakuwa kama yalivyoainishwa kwenye Fomu ya Dhamana ya Malipo ya Awali iliyotolewa katika Nyaraka Sanifu za Zabuni husika. |
| 19. | **Mapitio ya Mwongozo** | 19.1 Mwongozo huu utafanyiwa mapitio kila baada ya miaka mitatu au pale itakapohitajika. |

**KIAMBATISHO Na. 1: TAMKO LA DHAMANA YA UTEKELEZAJI WA ZABUNI**

Tarehe: [*weka siku, mwezi na mwaka)]*
*Namba na jina la mkataba: [ingiza nambari ya mkataba na jina]*

Mimi/Sisi tunakubali kwamba chini ya masharti na vigezo vya mkataba uliotajwa hapo juu, Mimi/Sisi tunawajibu wa kuhakikisha utekelezaji wa mkataba huo kwa uaminifu na [Mkandarasi/Muuzaji wa bidhaa/Mtoa Huduma/Mshauri elekezi] (chagua kinachofaa) kuhusiana na majukumu yote chini ya mkataba.

Mimi/Sisi tunakubali kwamba endapo tutashindwa kutekeleza mkataba kwa mujibu wa masharti na vigezo vilivyowekwa, Mimi/Sisi tunaweza kufungiwa kushiriki katika ununuzi wa umma kwa muda utakaobainishwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma, kwa mujibu wa Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura ya 410 na Kanuni zake

Tamko hili la dhamana ya utekelezaji wa mkataba litakuwa halali hadi hapo kazi itakapotekelezwa kikamilifu na kukubaliwa rasmi na Mwajiri/Mteja/Mnunuzi (chagua linalofaa).

Imetamkwa na kutiwa saini na:

Jina: [weka jina la mtu anayesaini Tamko la Utekelezaji wa mkataba]

Saini: [weka saini ya mtu ambaye jina na uwezo wake vimeonyeshwa]
Cheo: [weka cheo cha mtu mwenye nguvu ya kisheria anayesaini Tamko la Utekelezaji wa mkataba]

Ameidhinishwa rasmi kusaini Mkataba huu kwa niaba ya: [weka jina kamili la Mkandarasi/Mtoa Huduma/Mshauri elekezi/Muuzaji wa bidhaa (chagua inayofaa)].

Imesainiwa tarehe ... siku ya ... [weka tarehe ya kusaini].

**Kiambatisho Na. 2: Tamko la dhamana ya Uhifadhi wa Mazingira na jamii**

Tarehe: [*weka siku, mwezi na mwaka)]*
*Namba na jina la mkataba: [ingiza nambari ya mkataba na jina]*

[Weka jina kamili la Mwajiri/Mteja/Mnunuzi] (chagua inayofaa)
[Weka anwani kamili ya Mwajiri/Mteja/Mnunzi] (chagua inayofaa)

Tamko

Mimi/Sisi, tuliotia saini hapa chini, tunakubaliana kama ifuatavyo:

1. Uelewa wa Majukumu:

Mimi/Sisi tunakubali kwamba chini ya masharti na vigezo vya mkataba vilivyotajwa hapo juu, Mimi/Sisi tuna wajibu wa kuhakikisha uzingatiaji kwa uhaminifu wa dhamana ya Uhifadhi wa Mazingira na jamii na [Mkandarasi/Muuzaji/Mtoa Huduma/Mshauri elekezi] (chagua inayofaa) kuhusiana na majukumu yote chini ya mkataba.

2. Matokeo ya Kutotekeleza wajibu wa kimkataba:

Mimi/Sisi tunakubali kwamba endapo tutashindwa kutekeleza mkataba kwa mujibu wa masharti na vigezo vya Kimazingira na jamii vilivyowekwa, mimi/sisi tunaweza kufungiwa kushiriki katika ununuzi wa Umma kwa muda utakaobanishwa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma, kwa mujibu wa Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura ya 410 na Kanuni zake.

3. Uhalali wa Tamko:

Tamko hili la la Uhifadhi wa mazingira na jamii litakuwa halali hadi hapo kazi itakapotekelezwa kikamilifu na kukubaliwa rasmi na Mwajiri/Mteja/Mnunuzi (chagua linalofaa).

Imetamkwa na kutiwa saini na:
Jina: [weka jina la mtu anayesaini dhamana ya Uhifadhi wa Mazingira na Kijamii]

Saini: [weka saini ya mtu ambaye jina na uwezo wake vimeonyeshwa]
Cheo: [weka cheo cha mtu mwenye nguvu ya kisheria anayesaini dhamana ya Uhifadhi wa Mazingira na Kijamii]

Saini: [weka saini ya mtu ambaye jina na uwezo wake vimeonyeshwa]
Cheo: [weka nguvu ya kisheria wa mtu anayesaini dhamana ya Uhifadhi wa Mazingira na Kijamii]

Ameidhinishwa rasmi kusaini Mkataba huu kwa niaba ya: [weka jina kamili la Mkandarasi/Mtoa Huduma/Mshauri elekezi/Muuzaji wa bidhaa (chagua inayofaa)].

Imesainiwa tarehe ………... siku ya ……... mwaka………. [weka tarehe ya kusaini].

Weka
Muhur i/stempu ya kampuni (kama inavyofaa)